

# Kuhusu Help Me Grow

Help Me Grow ni mfumo wa huduma za usaidizi kwa wanawake wajawazito, walezi walio na watoto wachanga na familia zilizo na watoto wadogo wenye matatizo ya kuchelewa kukua na ulemavu.

Huduma na msaada hutolewa kupitia huduma za Ziara za Nyumbani na Msaada wa Mapema, ambazo yote husaidia familia na kuendeleza ukuaji na maendeleo bora ya watoto wachanga, watoto wadogo na familia zao.

Department of Children & Youth

Help Me Grow

*Huduma na msaada vinapatikana katika jimbo nzima na hutolewa na wataalamu wanaopatikana mahali ulipo.*

## Unganishwa na huduma za Ziara za Nyumbani au Msaada wa Mapema leo!

Jaza fomu ya ombi la huduma mtandaoni katika **www.helpmegrow.org.**

Piga simu kwa nambari **(800) 755-GROW (4769)** uzungumze na mtaalamu wa uandikishaji

Swahili: November 2024

# ZIARA ZA NYUMBANI



Department of Children & Youth

Help Me Grow

**www.helpmegrow.org**

# MSAADA WA MAPEMA



## Kulingana na takwimu...

**95%**

Zaidi ya **95%** ya wazazi katika jimbo la Ohio waliopata huduma ya Msaada wa Mapema kwa ajili ya watoto wao waliripoti kwamba waliweza kuwasaidia vyema watoto wao kujifunza mambo mapya na kupata ujuzi mpya.

Huduma za mpango wa Help Me Grow zinasaidia kukuza mahusiano, hali na mazingira bora ya kusaidia ukuaji wa ubongo, ambapo **80%** ya ukuaji huo hutokea kabla ya kufikisha umri wa miaka mitatu.

**80%**

**48%**

Wanawake wajawazito walioshiriki katika huduma ya Ziara za Nyumbani walikuwa na uwezekano wa **48%** wa kutopata watoto waliozaliwa na uzani wa chini.



# Msaada wa Mapema ni nini?

Msaada wa Mapema husaidia familia kuanzia wakati wa kujifungua watoto hadi umri wa miaka mitatu wenye matatizo ya kuchelewa kukua au ulemavu iii wawe na mwanzo bora katika maisha.

Wataalamu wa huduma ya Msaada wa Mapema hushirikiana na familia ya mtoto iii kutambua uwezo na mahitaji na kushughulikia masuala ya ukuaji mapema iwezekanavyo. Huduma hizi hutolewa mahali ambapo familia huishi, hucheza na kukaa.

Huduma ya Msaada wa Mapema inapatikana katika jimbo zima na kwa mtoto yeyote anayestahiki, bila kujali mapato ya familia.





# Ziara ya Nyumbani ni nini?

Ziara za Nyumbani ni huduma ya kujitolea ya nyumbani inayotolewa bila malipo kwa familia. Watoa huduma na wataalamu wa huduma ya ziara za nyumbani huunganisha wazazi kwa huduma za kupata maelezo na nyenzo zinazokuza afya ya watoto na familia nzima.

Huduma ya Ziara za Nyumbani inaweza kuboresha matokeo ya ujauzito na kusaidia familia kujiandaa kupata mtoto mchanga. Hata baada ya mtoto kuzaliwa, huduma ya Ziara za Nyumbani inaweza kusaidia familia kujifunza kuhusu kula, kulala na jinsi ya kudumisha usalama na ustawi wa watoto wao wachanga.